



Karibu sana katika tovuti hii ya *ndoto zangu* ili uweze kujifunza kwa kupitia ndoto uotazo...

Jina la Yesu Kristo lihimidiwe milele yote....

Maandiko yanasema Mungu anasema na sisi kupitia ndoto tuotazo,yawezekawa mara moja mpaka mara tatu kwa lengo la kuisisitiza ndoto hiyo...

Na ndoto nyingi huja kulingana na shughuli zetu nyingi na mihangaiko mingi ya siku nzima

Mhubiri 5:3

[3]Kwa maana ndoto huja kwa sababu ya shughuli nyingi; na sauti ya mpumbavu kwa njia ya wingi wa maneno.

Sasa ukiona umeota ndoto ya moto umewaka au umewasha moto,na imekuja kwa uzito kidogo yakupasa ufahamu maana ya ndoto hiyo kwa maana kuna jambo la kujifunza hapo..

Maandiko yanasema...

Yakobo 3:5-6

[5]Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu. Angalieni jinsi *moto* mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana.

[6]Nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwasha moto na jehanim.

Kuwa Makini na maneno yanayotoka katika kinywa chako,acha kuwasengenya watu na kuwazungumzia wengine vibaya...Ulimi ni moto ulojaa uovu mwingi usipojua jinsi ya



kuudhibiti...

Mkimbilie Kristo leo akusafishe dhambi zako kwa damu yake takatifu ili akupe uwezo wa kushinda mambo yote maovu....

Bwana wetu anakuja...